



Siku moja  
mamangu  
alinunua matunda  
aina tofauti.



Tulijiuliza, "Mama  
atatugawia  
matunda wakati  
gani?"



Baadaye, kakangu,  
Rahim, alijificha na  
kuyala matunda  
yote!



Tulisema kwa  
hasira, "Rahim ni  
mtukutu tena ni  
mchoyo. Lazima  
aadhibiwe."



Mama aligundua  
kuwa matunda  
yote yalikuwa  
yameliwa.  
Alikasirika sana.



Tulimtazama  
Rahim kwa ukali.



Nilimwuliza mama,  
"Je, utamwadhibu  
Rahim?"



Baadaye, Rahim  
alipata adhabu  
asiyoitarajia.



Hakuweza kutulia!



Mama  
alipomwuliza  
alijibu kwa sauti ya  
chini, "Naumwa na  
tumbo."



Hiyo ilikuwa  
adhabu mbaya  
kuliko kama Rahim  
angechapwa na  
mama.



Alipopata nafuu,  
Rahim alituomba  
msamaha. Aliahidi  
kuwa hataiba tena.